

Fahamu njia asili za kudhibiti wadudu sumbufu na magonjwa

Uzalishaji wa mboga mara nyingi unahusisha matumizi ya viuatilifu vyenye kemikali. Wakulima baadhi hawawezi kumudu gharama kubwa za viuatilifu hivi, ambavyo visipotumika vizuri – huweza kuleta madhara, kama kuharibu mazingira, mimea na kuathiri watumiaji wa mboga. SEVIA pia inahamasisha njia za asili katika kupambana na wadudu sumbufu na magonjwa bila kemikali.

Mchanganuo wa baadhi ya viuatilifu vya asili;

Jinsi ya kuandaa mchanganyiko wa mwarobaini

Majani ya mwarobaini ni kiuatilifu cha asili chenye uwezo wa kudhibiti wadudu kama vimamba, mbawakawa/kombamwiko, panzi, Funza/viwavi, mbawakawa wa kijapani, nzige, wadudu wenye magamba laini, chawa/vithiripi, fukusi, utitiri na nzi weupe.

Ponda kilo 2 za majani ya mwarobaini na weka katika chombo chenye mfuniko. Ongeza lita 2 za maji, funika vizuri na uache kwa siku 3. Chuja kupata mchanganyiko wako. Chukua lita moja kutoka kwenye mchanganyiko wa lita mbili na uchanganye na lita 9 za maji. Ongeza mili lita10 za sabuni iliyoyeyushwa, koroga vizuri na nyunyiza kwenye mimea iliyoathiriwa.



Jinsi ya kuandaa mchanganyiko wa mchaichai

Mchaichai una ufanisi mkubwa wa kuzuia magonjwa ya ukungu na bakteria kwenye mboga mboga.

Ponda gramu 50 za mchaichai, uloweka ndani ya lita mbili za maji kwa usiku mzima. Chuja mchanganyiko huo na kuuweka moja kwa moja kwenye bomba la kunyunyiza (zidisha mchanganyiko wa maji na mchaichai kiasi cha mara mbili au tatu kulingana na wingi wa mazao yako). Nyunyiza mchanganyiko huo mara moja kwa wiki. Rudia tena kama kuna ulazima.



Jinsi ya kuandaa majani ya basili/mfumbasi

Majani ya basili/mfumbasi yana ufanisi mkubwa dhidi ya viwavi, nzi wa matunda, utitiri wekundu, utitiri weupe, wadudu wenye magamba laini, kombamwiko wa madoa, magonjwa ya fangasi na minyoo fundo.

Ponda gramu 50 za majani ya basili/mfumbasi na loweka ndani ya lita mbili za maji kwa usiku mzima. Tmia chujio kumimina mchanganyiko huo ndani ya bomba la kunyunyiza pamoja na mililita 10 za mchanganyiko wa sabuni na koroga vizuri. Tumia mara moja kwa wiki, rudia tena kama kuna ulazima



Jinsi ya kuandaa mchanganyiko wa sabuni:

- Kata kipande kimoja cha sabuni
- Yeyusha katika lita moja ya maji
- Hifadhi mchanganyiko huo katika chombo maalumu

NB: Mchanganyiko huu wa sabuni pia unafaa dhidi ya vimamba au inzi weupe, unapoyunyizwa.

Jinsi ya kuandaa kitunguu swaumu

kitunguu swaumu pia kinaweza kuwa mbadala wa kudhibiti viwavi, nzi wa matunda, utitiri wekundu, utitiri weupe, wadudu wenye magamba laini, kombamwiko wa madoa, magonjwa ya fangasi na minyoo fundo.

Menya kilo mbili za kitunguu swaumu na uzitwange vizuri (tumia blenda ni vizuri zaidi). Ongeza mililita 500 za maji ili kusaidia kukamua juisi/mchanganyiko. Tumia chujio kupata mchanganyiko wa kitunguu swaumu. Weka kwenye chupa au chombo maalumu na ongeza maji kutengeneza lita 10 za mchanganyiko. Weka mchanganyiko huo kwenye chombo kilichofunikwa. Weka alama kwenye chombo hicho. Kwenye mchanganyiko wa lita 10, toa lita moja na weka kwenye bomba la kunyunyiza, ongeza lita 15 za maji ili kukamilisha tanki zima, na ongeza mililita 10 za sabuni kimiminika. Nyunyiza wakati wa asubuhi au jioni kwenye mimea iliyoathiriwa. Nyunyiza kila baada ya wiki moja. Mchanganyiko huo unaweza kutumika ndani ya miezi 3.

Jinsi ya kutengeneza mchanganyiko/mchapulo wa viuatilifu asili

Mchanganyiko huu unaweza kutumika kudhibiti wadudu wanaofyonza na kutafuna

Kata kata vipande vidogo vya mimea ifuatayo: kilo 1 ya majani ya mwarobaini, gramu 500 za kitunguu swaumu, gramu 500 za tangawizi, mimea 5 ya mchaichai na majani mabichi 5 ya tumbaku. Chemsha mchanganyiko kwenye lita 20 za maji. Changanya wakati wa kuchemsha, ongeza vipande vya sabuni vilivyosagwa kwenye mchanganyiko huo. Baada ya kuchemsha, acha mchanganyiko huo upoe.

Tumia chujio kuchuja mchanganyiko huo na kuweka kwenye chombo maalumu. weka mililita 450 za kiuatilifu asili kwenye maji lita 16, nyunyiza wakati wa asubuhi au jioni kila baada ya wiki moja. Mchanganyiko huu unaweza kutumika ndani ya miezi 3.